



Kuna uwezekano kwamba kutakuwa na watu ambao watatusaidia kumtunza mtoto wetu. Wale wanaotoa huduma wanaweza kuwa na matarajio yasiyo halisi kwa watoto au wanaweza kukosa mafunzo na uzoefu katika kuwatunza watoto. Usifikiri kwamba walezi wanajua matarajio yako, ni jukumu lako kuwaeleza kwa uwazi.

KILE AMBACHO MLEZI ANAHITAJI KUJUA

Kukabiliana na Kulia

- Mwonyeshe mlezi jinsi ya kumtuliza mtoto wako.
- Muweke mtoto mahali salama na upige simu mara moja ikiwa mtoto hataacha kulia.
- Jadili kile ambacho mtoto anapenda kufanya na midoli ya kuchezea ambayo anaipenda.

Usingizi Salama

- Mtoto anapaswa kulala peke yake na kamwe asilale na mtu mzima au mtoto mwingine.
- Mtoto anapaswa kulala kwa mgongo kila wakati kwenye kitanda cha mtoto/basineti/kitanda kinachobebeka na kamwe asilale kwenye matandiko laini, blanketi, au mito.

Usalama wa Maji

Daima mwangalie mtoto akiwa kwenye beseni la kuogea, bwawa la kuogelea, vyanzo vya maji au vitu vingine vilivyojaa maji, ikiwa ni pamoja na vyoo.

NI NINI UNAWENZA KUFANYA?

Unapoondoka Nyumbani

- Mwachine mlezi nambari yako ya simu na nambari nyingine za dharura.
- Mjulisha mlezi kwamba ni sawa kukupigia simu kwa ajili ya msaada. Wasiliana na walezi ukiwa mbali.

Unapofika Nyumbani

- Muulize mlezi alifanya nini wakati ulikuwa mbali.
- Baada ya mlezi kuondoka, muulize mtoto ikiwa alimpenda.
- Angalia tabia ya mtoto anaporudi nyumbani. Je, mtoto anaonekana kuwa na amani na furaha?
- Ikiwa unashuku kuna shida au ikiwa ameumizwa, tafuta msaada mara moja.

Kuvisha Nepi/Kutumia Choo

- Watoto hujichafua wanapojaribu kutumia vyoo, ni jambo la kawaida na linatarajiwa.
- Kuwa na nepi za ziada na nguo safi ili kumbadilisha kadri inavyohitajika.

Kula


- Jadili utaratibu wa ulishaji, ikiwa ni pamoja na kiasi ambacho kwa kawaida mtoto hula.
- Kujichafua kwa chakula ni jambo la kawaida na linalotarajiwa. Hakikisha vifaa vya kufanyia usafi vinapatikana.

Nidhamu

- Kamwe usimpige makofi, kumkaripia, kumrushia vitu, kumtikisa au kumgonga mtoto.
- Wafundishe watoto tabia zinazokubalika.

PATA MAELEZO ZAIDI

Tazama broshua nzima kwa kuskani hapa chini.



Mfundishe Mtoto Wako

- Jina la jirani anayeaminika la kumpigia simu au kwenda kwake ikiwa anahisi yuko hatarini.
- Jinsi ya kupiga simu "911" wakati wa dharura.
- Ni sawa kuzungumza ili kujadili na wewe matatizo au wasiwasi ambao anaweza kuwa nao kuhusu mlezi.